

## **SHULE BORA KUWANOA VIONGOZI NA WALIMU WA SOMO LA KINGEREZA HALMASHAURI YA WILAYA YA CHEMBA**

Programu ya Shule Bora imeanza Mafunzo ya kuwajengea uwezo Maafisa Elimu Kata,Wakuu wa Shule na Walimu wa Somo la Kingereza ili kuhakikisha Shule zao zinafanya vizuri zaidi katika somo hilo.

Mafunzo hayo yamefanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Kondoa Irangi ambapo yamefunguliwa na Kaimu Mkurugenzi Elimu TAMISEMI Bi. Suzan Nussu.

“Tarajio langu ni kuona baada ya kupata Mafunzo haya tupate Mrejesho wa kuona Walimu wamepata Umahiri baada ya kujengewa uwezo wa Mafunzo mliyoyapata na Agizo la TAMISEMI ni kuona Shule zilizojengewa uwezo zinafanya vizuri”.Amesema Bi Suzan.

Bi. Suzan ameongeza kuwa Nia ya Serikali ni kuhakikisha Somo la Kingereza linajengewa uwezo kwa watoto wa Darasa la kwanza kupitia Mtaala mpya ili wawe Mahiri wakati watakapokua Sekondari.

Kwa upande wake Afisa Elimu Mkoa Mw.Vicent Boniface Kayombo amesema Serikali imejipanga kwa kuendelea kufanya Uwekezaji Mkubwa kwa Walimu wake wa kuwawezesha kupata Umahiri.

Mw.Vicent ametoa rai kwa Maafisa Elimu kata na Walim Wakuu Shule za Msingi baada ya kupata Mafunzo hayo kuwa Wakufunzi kwenda kuwafundisha wengine na kuona Matarajio mazuri kwenye utekelezaji wa Majukumu yao.

Bi.Asia Mashaka Mwezeshaji Mkuu wa Mafunzo amesema Lengo kuu la Mafunzo hayo ni kuwajengea uwezo Walimu wa Shule za Msingi kuweza kutengeneza Mtaala ulioboreshwa katika somo la Kingereza.

“Matarajio yetu ni kuona Viongozi hawa watajadili Mabadiliko ambayo yametokea katika Mtaala ulioboreshwa ,Kubaini mabadiliko ambayo yamefanyika katika Muhtasari wa Somo la Kingereza ,kufanya Mjadala wa pamoja kuona namna ya Ufundishaji unavyofanyika huko Shuleni kwenye Somo la Kingereza ,Kuandaa Mpango kazi wa namna watakavyoenda kuwawezesha walimu”.Amesema Bi Asia.

Akiongea awali Afisa Elimu Taaluma Mkoa wa Dodoma Mw. Jeni Aman amewapongeza washiriki kwa kupata mafunzo hayo ili waweze kusimamia vizuri watakachojifunza Walimu wa Kingereza.

Mafunzo ya kuwajengea Uwezo Walimu wa Somo la Kingereza yanafanyika kwa Halmashauri ya Wilaya ya Chemba ambapo siku ya kwanza Viongozi wa Elimu ya Awali na Msingi ngazi ya Wilaya Maafisa Elimu kata na Walimu Wakuu wanashiriki na kuanzia tarehe 21-25 Walimu 100 watapatiwa mafunzo kutoka kwa Wawezeshaji kutoka Taasisi ya Elimu Tanzania ,Chuo cha Ualimu Marangu, Udhhibiti Ubora wa Shule Muheza pamoja na Ofisi ya Kamishna wa Elimu.